MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 03/12/2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA

KU/SMC/BM/70/2021 – WALIOHUDHURIA:

A. WAHESHIMIWA MADIWANI

1.	Mhe. Jastin Malisawa	-	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Mhe. Istus Kapufi	-	Naibu Meya
3.	Mhe. Dimela Kafwa	-	Diwani viti Maalum
4.	Mhe. Juma Mnanka	-	Diwani Kata ya Msua
5.	Mhe. Adorfina Konongo	-	Diwani Kata ya Lwiche
6.	Mhe. Frank Lupimo	-	Diwani Kata ya Milanzi
7.	Mhe. Francis Manyika	-	Diwani Kata ya Majengo
8.	Mhe. Mary Kipalasha	-	Diwani Kata ya Malangali
9.	Mhe. Hadija Maufi	-	Diwani Viti Maalum
10.	Mhe. Edwin Misasi	-	Diwani Kata ya Katandala
11.	Mhe. Roswita Chekwe	-	Diwani Viti Maalum
12.	Mhe. Janeth Sinyangwe	-	Diwani Viti Maalum
13.	Mhe. Colnel Kafumu	-	Diwani Kata ya Sumbawanga
14.	Mhe. Anthony Kayombo	-	Diwani Kata ya Chanji
15.	Mhe. Gabriel Kimamala	-	Diwani Kata ya Izia
16.	Mhe. Charles Chakupewa	-	Diwani Kata Ya Momoka
17.	Mhe. Andrea Cheka	-	Diwani Kata ya Kizwite
18.	Mhe. Juma Dawood Nzegere	-	Diwani Kata Mazwi
19.	Mhe. Agustino Ngoani	-	Diwani Kata ya Ntendo
20.	Mhe. Syriacus Pangani	-	Diwani Kata ya Kasense
21.	Mhe. Cardius Mtullo	-	Diwani Kata ya Pito
22.	Mhe. Leticia Kipeta	-	Diwani Viti Maalum
23.	Mhe. Sangu Maarifa	-	Diwani Kata Mollo
24.	Mhe. Anna Mwamba	-	Diwani Viti Maalum
25.	Mhe. Lameck Pondamali	-	Diwani Kata ya Mafulala

B. WATAALAM

1.	Ndg. Jacob J. Mtalitinya	-	Mkurugenzi wa Manispaa Katibu
2.	Ndg. Frank Mateni	-	Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii
3.	Ndg. Andrew Zumba	-	Afisa Uchaguzi
4.	Ndg. Victor Ndziku	-	Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika
5.	Ndg. Ardius Kwimba	-	Kaimu Mchumi Manispaa
6.	Ndg. Joseph Nkonjera	-	Afisa Misitu
7.	Ndg. Cecilia Kasambasha	-	Kaimu Afisa Utumishi na Utawala

8. Ndg. Thadeo Maganga - Afisa Maliasili na Utalii
9. Ndg. George Nyanga - Afisa Usafirishaji
10. Ndg. Deogratius Masalu - Kaimu Mkaguzi wa Ndani
11. Ndg. Peter Tarimo - Afisa Elimu Msingi
12. Ndg. Mussa Nginila - Afisa Manunuzi
13. Ndg. Fortunatus C. Lyapa - TSC
14. Eng. Denis Eliakimu - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi
15. Ndg. Jenifrida Manuma - Afisa TEHAMA
16. Ndg. James Mawkinya - Mwanasheria Manispaa
17. Ndg. Salustian Shirima - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika
18. Ndg. Oswald Temba - Afisa Afya
19. Dr. Sebastian Siwale - Kaimu Mganga Mkuu
20. Ndg. Richard Mkandarasi - Kaimu Afisa Biashara Manispaa
21. Ndg. James Kajungu - Kaimu Afisa Mipango Miji
22. Ndg. Muyemba - Kaimu Afisa Mazingira

C: WAALIKWA

1. Ndg. Sebastian Waryuba - Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga
2. Ndg. Neema Fungo - Jeshi la Akiba
3. Ndg. Sabina Mwajeka - Afisa Tarafa Itwelele
4. Ndg. Dafroza Msechu - Afisa Tarafa Lwiche
5. Ndg. Mohamed Mlumba - UHAMIAJI
6. Ndg. J. Mollel - Afisa Usalama Wilaya
7. SSP Maria D. Kway - Mkuu wa Polisi Wilaya
8. Ndg. Christina Mzena - DAS
9. Ndg. Melkior Komba - Magereza
10. Ndg. Tabu Shaaban - Katibu CCM Wilaya
11. Ndg. Chami Chasuka - Mwenyekiti CCM
12. Ndg. Elizabeth Simkway - Afisa Serikali za Mitaa
13. Ndg. Ndg. James Mbungano - TAKUKURU
14. Ndg. Baraka Lusajo - ITV
15. Ndg. Sammy Kisika - AZAM TV
16. Ndg. Edith Peter - VOS
17. Ndg. Misri Mwasenga - STAR TV
18. Ndg. Peter Helatano - Global TV
19. Ndg. Musa Mwangoka - Mwananchi
20. Eng. Samson Kelesi - TARURA
21. Eng Emmanuel Kudema - TARURA

D. SEKRETARIETI

1. Ndg. Khadija Dalasia - Katibu wa Vikao

KU/SMC/BM/71/2021 – KUFUNGUA KIKAO:

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, Mwenyekiti alianza kwa kusoma dua. Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kutufikisha siku ya leo ambapo alisema kuwa kikao cha leo ni kikao cha Kawaida cha robo . aliomba wajumbe wazingatie kanuni katika kuchangia hoja katika kikao hiki. Mwenyekiti Alifungua kikao mnamo saa 4.17 Asubuhi

KU/SMC/BM/72/2021 – KUTHIBITISHA DONDOO:
Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 03.12.2021 wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzithibitisha.

KU/SMC/BM/73/2021 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MSTAHIKI MEYA NA MKURUGENZI

Swali
Mhe. Chakupewa alipenda kufahamu ni kwanini Chuo cha Veta hakijakamilika kwa wakati na je lini sasa Chuo hicho kitakamilika

Jibu
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa ujenzi wa Chuo cha Veta ulisamama kwasababu fedha za kumalisha chuo hicho zilikuwa hazijaletwa sasa wanasubiri fedha zije zikifika ukamilishaji wa chuo hicho utaendelea.

Swali
Mhe. Chakupewa alipenda kufahamu ni lini gari la Mstahiki Meya litapokelewa?

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa kwasasa wanaendelea na taratibu za manunuzi na taratibu hizo zitakapokamilika magari hayo yanaweza kupokelewa ifikapo Mwezi Januari 2022.

Swali
Mhe. Andrea Cheka alipenda kufahamu ni lini Mzabuni atamaliza kuzoa takataka zilizopo chini.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Mzabuni kwa sasa anaendelea na zoezi la uzoaji taka japo Magari ya kuzolea taka yalipata changamoto ila tumeshapata kifaa na

gari linatengenezwa hivyo ndani ya muda mfupi takataka zote zitakuwa zimeondolewa.

Swali
Mhe. Andrea Cheka alipenda kufahamu ni lini Halmashauri itanunua Magari mapya kwa ajili ya kuzoa takataka

Jibu
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa wamelipokea ombi hilo la ununuzi wa gari na wataliweka katika bajeti zinazokuja

KU/SMC/BM/74/2021 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 31.08.2021
Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa Marekebisho Ukurasa wa 1 kisha Katibu na Mwenyekiti waliuwekea saini Muhtasari huo.

KU/SMC/BM/75/2021 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 31.08.2021

Iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kiko cha tarehe 31.08.2021 wajumbe walipongeza utekelezaji wake.

KU/SMC/BM/76/2021 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA JULAI- SEPTEMBA 2021.

A. KAMATI YA UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati ya UKIMWI aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya UKIMWI kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2021 . Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

Hoja
Mhe. Cheka alipenda kufahamu ni nini kifanyike ili kumaliza wimbi la watoto wa mitaani

Jibu
Mwenyekiti aliwaambia wajumbe hii ni hatua ya kwanza ya kuwatambua hawa watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili watapowakamatwa na wanaweza kupelekwa katika vyuo vya Ufundi kama vile VETA na Katandala .

Taarifa ilipokelewa

B: KAMATI YA UCHUMI AFYA NA ELIMU

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi Afya na Elimu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Uchumi Afya na Elimu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2021 . Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

Hoja

Mhe. Cheka alipenda kufahamu ni kigezo gani kinatumika kutambua shule kongwe na shule zisizokuwa kongwe

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa Halmashauri ina mfumo wa takwimu unaoeleza kila shule ilianza lini na changamoto zake na hapo ndio utapata shule kongwe na uhaba wa miundo mbinu kwa kila shule

Hoja

Mhe. Ngoani alipenda kufahamu ni kwanini vikundi katika Kata za Vijijini hawapewi Mikopo ya 10%

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa vikundi vyote katika Kata zote zitaguswa kulingana na sifa za vikundi vinavyotakiwa kukopeshwa

Tarifa ilipokelewa

C: KAMATI YA MIPANGO MIJI

Mwenyekiti wa kamati ya Mipango Miji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Mipango Miji kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2021, Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

Hoja

Mhe. Dimela Kafwa alipenda kufahamu ni lini waliopewa viwanja wataviendeleza?

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa kulingana na sheria ya Mipango Miji Mwananchi aliyepewa kiwanja atatakiwa kukiendeleza kiwanja alichopewa ndani ya Miaka 3 , kwa sheria hii wananchi waliopewa viwanja katika Maeneo tuliyoyapima ya Isofu, Katumba hawajamaliza miaka 3, kipindi hicho kikiisha na wakawa hawajaviendeleza basi watanyang'anywa kwa mujibu wa sheria

Taarifa ilipokelewa

C: KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI

Mwenyekiti wa kamati ya Fedha na Uongozi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba 2021, Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

Hoja

Mhe. Mtullo alipenda kufahamu ni lini vibarua wa stendi ya Katumba Azimio watalipwa posho zao za kila Mwezi kwani wanadai kwa muda mrefu hali inayopelekea upotevu wa mapato?

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa kuna Madeni katika Halmashauri yetu na taarifa yake ataitoa katika taarifa ya Mstahiki Meya japo tumewshaweka mikakati ya kuanza kulipa Madeni haya.

Hoja

Mhe. Dimela Kafwa alipenda kufahamu ni lini ziara ya Waheshimiwa Madiwani itafanyika ili waweze kupata uzoefu katika kutekeleza majukumu yao

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa tunaendelea kuomba kibali cha ziara kwa Mkuu wa Mkoa na tukipata kibali hicho na hali ya Mapatao ikikaa vizuri basi Baraza la Madiwani litakwenda kujifunza

Hoja

Mhe. Chakupewa alipenda kufahamu ni kwanini Majengo ya Shule ya Msingi Momoka hayakufunguliwa na Mbio za Mwenge hali iliyofifisha nguvu za wananchi.

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa utaratibu wa Mbio za Mwenge huwa na Kamati Nyingi zinazoamua ni miradi gani itazinduliwa au kupitiwa na Mwenge , hivyo Mhe. aendelee kuwa na miradi ya kutosha katika Kata yake na kuna siku Mwenge utafika katika eneo lao

Hoja

Mhe. Kimamala alipenda kufahamu ni lini Kikao maalum cha Kamati ya fedha na Uongozi kiujadili Mapato kitafanyika

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa wamekubaliana kuwa kikao hiki kifanyike kabla ya vikao vya bajeti ili tuweze kujadili kwa kina mwenendo wa mapato katika Halmashauri yetu

Hoja

Mhe. Cheka alipenda kufahamu ni lini fedha za ruzuku zitapelekwa katika WDC zetu ili tuweze kuitisha vikao.

Jibu

Mwenyeki aliwambia wajumbe kuwa kuanzia Mwezi Julai 2021 Halmashauri hazijapokea fedha kwa ajili ya ruzuku kwa maana ya GPG hivyo pindi fedha hizo zitakapokuja basi watapeleka na kwenye Kata

Taarifa Ilipokelewa .

KU/SMC/BM/77/2021 TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatailiaji aliwasilisha taarifa ya Utekelezaji kazi Miaradi ya maendeleo kipindi cha robo ya kwanza ya julai- Septemba 2021, wajumbe walichangia kama ifuatavyo:

Hoja

Mhe. Andrea Cheka alipenda kufahamu ni lini ukamilishaji wa shule ya msingi Senti utawekwa kwenye bajeti

Jibu

Afisa Mipango aliwaambia wajumbe kuwa Bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa Shule ya msingi Senti ilikuwepo katika bajeti ya Mwaka 2020/2021 ila fedha hazikuletwa hata hivyo katika bajeti ya Mwaka 2022/2023 wataweka bajeti kupitia EP4R kwa ajili ya kukamilisha Madarasa katika shule hiyo.

Hoja

Mhe. Mtullo alipenda kufahamu ni lini miradi ya shule ya msingi Katumba na Itwelele Sekondari itakamilishwa

Jibu

Afisa Mipango aliwaambia wajumbe kuwa Miradi hiyo ipo katika bajeti ya Mwaka 2021/2022 kupitia EP4R.

Hoja
Mhe. Juma Dawood alipenda kufahamu ni lini Halmashauri itatoa Mikopo ya 10 % kwa Vikundi vya Wanawake , vijana na Watu wenye Ulemavu.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa tarehe 09/12/2021 Mkipo itatolewa kwa Vikundi vya Vijana, Wanawake na watu wenye Ulemavu na tutatoa mikopo ya Bajaj, Pikipiki na fedha kwa baadhi ya vikundi.

Mwenyekiti aliomba wajumbe wapate muda na wafike Ofisi ya Mchumi kujua ni miradi gani inatekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Taarifa Ilipokelewa.

KU/SMC/BM/78/2021 – TAARIFA YA MSATHIKI MEYA

1. **TAARIFA KUHUSU MADENI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA**

Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa Halmashauri inadaiwa madeni mbalimbali kama Ifuatavyo:

- Madeni ya Watumishi - 1,568,783,459.00
- Madeni ya Wazabuni - 959,715,244.00
- Madeni ya Wakandarasi - 3,069,075,626.00

Aliwaambia wajumbe kuwa kama Halmashauri kuna hatua tumeanza kuzifanya kupunguza madeni haya na kwa kuanzia kuna timu ina hakiki madeni haya na katika bajeti yetu ijayo tutaweka asilimia 30 ya mapato yetu ili tuweze kulipa madeni hayo.

Alisema kuwa wameona watoe taarifa hii ili Waheshimiwa Madiwani waweze kujua Ukubwa wa Madeni katika Halmashauri yetu na pia kama kuna Changamoto au kuna utata wanakutana nao huko wakati wa utekelezaji wa majukumu yao nasi wasisite kufika katika ofisi ya Mstahiki Meya na Mkurugenzi kwa ufafanuzi kuhusu jambo hili.

2. **TAARIFA YA MIRADI YA TACTICS**

Mstahiki Meya aliwasilisha Taarifa ya Miradi ya TACTICS ambayo tunatarajia kuanza kutekeleza katika Mwaka ujao ambapo tutaanza na Ujenzi wa Soko na Ujenzi wa Barabara Km 13 na barabara zilizopitishwa ni

- Barabara ya Mwaiseni Km 0.4
- Barabara ya Sokolo – Bible Km 2.6

- Mtaa wa Kalangasa Km 0.5
- Mtaa wa Kasema Km 0.4
- Mtaa wa Maendeleo Km 0.2
- Sido – Senga – Mafulala Km 1.2
- Muva Km 0.2
- Regional Block – Msakila Km 1.2
- Kimati – Ufipa Km 0.2
- Airport – Senga –Wipanga Km 3.0
- Kuzunguka Hospitali ya Isofu Km 2.0 (Ombi Maalum)
- Kuzunguka soko la Mazao Kanondo Km 2.0 (Ombi Maalum)

Wajumbe waliipokea taarifa hii na kupongeza juhudi na jitihada zinzofanyika katika kuboresha Mji wetu

Saalm za Chama Cha Mapinduzi Wilaya

Mwenyekiti wa Chama aliomba Halmashauri ihakikishe Ilani ya Chama Tawala inatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo kila mmoja kwenye sekta yake awajibike kutekeleza Ilani ya Chama

KU/SMC/BM/51/2021 – KUFUNGA KIKAO:
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kuiletea maendeleo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mwenyekiti aliwashukuru kwa kusema wajumbe wameshiriki kikamilifu kwa kuwa wamekuwa wazi katika kuchangia hoja nyingi zenye tija. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 5.40 Asubuhi

Umesambazwa na ……. Saini ……. Tarehe ……

UMETHIBITISHWA / HAUKUTHIBITISHWA

……... ……..
Jacob J. Mtalitinya Mhe. Jastin Malisawa
Mkurugenzi Manispaa **Mstahiki Meya**
KATIBU **MWENYEKITI**